TATHMINI YA ELIMU YA MSINGI YA KENYA

SHUGHULI ZA DISEMBA 2026

GREDI YA 5 – SHUGHULI YA KISWAHILI KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Muda: Dakika 15 Kila Mwanafunzi

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina: _____ Shule: _____

Nambari ya Tathmini/UPI: _____ Tarehe: _____

Maelekezo kwa Wanafunzi

1. Andika jina lako, Nambari yako ya Tathmini/UPI na tarehe katika nafasi ulizopewa.
2. Kagua karatasi ya maswali kwa makini ili kuhakikisha kurasa zote zimechapishwa na hakuna swali lililoachwa.
3. Jibu maswali yote katika nafasi ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SEHEMU	ASILIMIA YA ALAMA	Amezidi Matarajio	Ametimiza Matarajio	Anakaribia Kutimiza Matarajio	Bado Hajafikia Matarajio	Maoni ya Mtathmini
KIWANGO CHA ALAMA (Kati ya 50)		**38–50**	**20–37**	**11–19**	**1–10**	
ALAMA ZA MWANAFUNZI						
KIWANGO		**4**	**3**	**2**	**1**	
WEKA ALAMA (✓)						

KAZI YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA Alama 10

Mada: Afya na Usafi wa Mwili

Maelekezo kwa Mwalimu

Soma kifungu hiki **mara mbili**. Wanafunzi wasikilize kwa makini bila kuona maandishi. Baada ya kusoma, waulize maswali yafuatayo kwa mdomo.

Kifungu cha Kusoma

Kila asubuhi, Baraka huamka mapema na kujiandaa kwenda shuleni. Baada ya kuamka, yeye hunawa uso, hupiga mswaki na kuoga. Mama yake humkumbusha kuvaa nguo safi na kuchana nywele vizuri. Baraka pia hupenda kunawa mikono kabla ya kula na baada ya kutoka chooni. Shuleni, mwalimu wake huwafundisha wanafunzi umuhimu wa kudumisha usafi wa mwili. Baraka anaamini kuwa mtu anayezingatia usafi huwa na afya njema na hujiamini anapokuwa pamoja na wengine.

Maswali ya Mdomo **(Alama 2 kila swali)**

1. Baraka huamka wakati gani?